JamiiYETU

11 MANISPAA ILEMELA INASTAHILI CHANZO KINGINE CHA MAJI

14 RANCHI NDOGO KIBITI ZAPUNGUZA MIGOGORO YA WAKULIMA, WAFUGAJI

Uwekezaji wabadili huduma za afya mpakani Tanzania, Msumbiji



Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliyojengwa katika Kijiji cha Mpitimbi jirani na nchi ya Msumbiji.



Serikali chini ya Rais Dk Samia Suluhu Hassan imeboresha huduma za afya na kupunguza vifo vya wajawazito kwa asilimia 80.

Na Albano Midelo

SAFARI ya kilometa nyingi kwa ajili ya matibabu sasa inaanza kuwa historia kwa wananchi wa Mpitimbi wilayani Songea mkoani Ruvuma na maeneo jirani ya nchi ya Msumbiji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Elizabeth Gumbo anasema zaidi ya Sh bilioni 3.17 zilizowekezwa Mpitimbi zimeanza kubadilika kutoka fedha za umma kuwa huduma za matibabu zinazogusa maisha ya watu.

Kutoka safari ndefu hadi huduma karibu

Miaka kadhaa iliyopita, baadhi ya wananchi wa maeneo ya Muhukuru na Mpitimbi walilazimika kuelekea Songea mjini au Peramiho kutafuta huduma ambazo hazikupatikana karibu.

Safari hizo zilimaanisha nauli, chakula, malazi, kupoteza siku za kazi na wakati mwingine kuchelewa kupata huduma muhimu na kusababisha vifo.

Mkazi wa Namatuhi, Sophia Haule anasema uwekezaji huo umebadili mtazamo wa wananchi kuhusu upatikanaji wa huduma za afya.

“Nainua sauti ya moyo wa shukrani kwa serikali kwa sababu Kata ya Mpitimbi haikuwahi kuwa na ndoto ya kujengewa hospitali kubwa ya wilaya,” anasema.

uk.12

Uwekezaji wabadili huduma za afya mpakani Tanzania, Msumbiji

INATOKA UK.9

Hospitali inayosogeza huduma za kibingwa

Taarifa ya Wizara ya Afya inaonesha Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliyopo Mpitimbi ilifunguliwa Juni 15, 2021 na sasa uwezo wake umeongezwa kwa miundombinu, vifaatiba na wataalamu hivyo kutoa pia huduma za kibingwa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mpitimbi, Dk Sakina Komesha anasema hospitali inatoa huduma za X-ray, upasuaji, macho, meno na huduma za uzazi ikiwemo upasuaji wa akina mama.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Dk Zaituni Hamza anasema uwekezaji katika miundombinu, vifaa na wataalamu umeongeza uwezo wa hospitali hiyo kutoa huduma za uchunguzi na matibabu kwa makundi mbalimbali ya jamii wakiwemo watoto.

Mabadiliko yanapimwa kwa maisha

Mkazi wa Kijiji cha Nambendo, Fatuma Umbala anasema alipofikisha mgonjwa kwa ajili ya kujifungua katika hospitali hiyo, alipokewa na kuhudumiwa haraka, huku wahudumu wakiendelea kufuatilia hali yake hadi kuimarika.

Hata hivyo, ameomba idadi ya watumishi wa afya katika hospitali hiyo iongezwe ili huduma ziendelee kuimarika.

Kwa Cathibet Mapunda ambaye ni mkazi wa Mpitimbi aliyekuwa na changamoto ya usikivu, anasema thamani ya hospitali imeonekana kupitia huduma za kibingwa.

Anasema madaktari bingwa waliowasili hospitalini hapo walimsaidia kupata matibabu yaliyorejesha hali yake ya usikivu kuwa ya kawaida.

Mmoja wa madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Rajabu Mtiula anasema wananchi wa kata saba za Jimbo la Peramiho katika Tarafa ya Muhukuru sasa wana fursa ya kutumia hospitali hiyo.

Kwa mujibu wa diwani huyo, huduma za afya zinazotolewa katika hospitali hiyo pia zina umuhimu kwa wananchi kutoka nchi jirani ya Msumbiji wanaovuka eneo la mpaka wa Mkenda.

Uwekezaji unaokutana na sera ya taifa

Mwelekeo huo unaendana na vipaumbele vya Wizara ya Afya vya kuboresha hospitali za ngazi zote, kuwekeza katika miundombinu, vifaa, dawa na wataalamu huku ukisisitiza huduma za afya ya mama na mtoto.

Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2023 iliyopitishwa na Bunge Novemba 2023 na kuidhinishwa na Rais Novemba 19, 2023, inalenga kupunguza vikwazo vya kifedha katika upatikanaji wa huduma.

Hivyo, hospitali kama Mpitimbi ni sehemu ya nguzo mbili zinazopaswa kwenda pamoja ambazo ni huduma ziwe karibu pamoja na wananchi kuwa na uwezo wa kulipia gharama kupitia mifumo endelevu ya bima.

Hospitali ya Mpitimbi kama kipimo cha maendeleo

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 inaweka matarajio ya Tanzania yenye huduma za afya bora, nafuu, jumuishi na zinazopatikana kwa usawa huku ikisisitiza teknolojia, miundombinu na rasilimali watu.

Dira hiyo inalenga pia Tanzania yenye mfumo imara wa afya unaoweza kulinda wanawake, watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

Hospitali inapokuwa na X-ray, upasuaji, huduma za macho, meno na uzazi, pengo kati ya sera na maisha ya kila siku linaanza kupungua.

Kwa nini uwekezaji huo ni muhimu

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani WHO, makadirio ya mwaka 2023 yanaonesha Tanzania ilikuwa na kiwango cha vifo vya uzazi cha 276 kwa kila vizazi hai 100,000.

Hata hivyo, Tanzania imepata maendeleo makubwa katika uboreshaji wa kwa mujibu wa Wizara ya Afya, kiwango cha vifo vya uzazi nchini Tanzania kimepungua kwa takribani asilimia 80 kutoka vifo 556 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000 kati ya mwaka 2015 na 2022.

Kwa mujibu wa Wizara ya afya, vifo vya watoto chini ya miaka mitano, vimepungua kutoka 67 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1,000, upatikanaji wa huduma kati ya asilimia 80 hadi 85 ya wananchi sasa wanapata huduma za afya ya uzazi na mtoto ndani ya kilometa 5 kutoka wanapoishi.

Serikali imeweka lengo la kushusha vifo vya uzazi kufika chini ya 70 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2030/2031.

Gharama ni sehemu ya ubora

Ukaribu wa hospitali unapunguza gharama zisizoonekana katika takwimu za hospitali, usafiri, muda, malazi na kipato kinachopotea.

Hivyo, kusogeza huduma karibu na wananchi na kupanua bima kunaweza kuwa sehemu ya mkakati wa kupunguza mzigo wa kifedha.

Kutoka mradi hadi matokeo

Changamoto inayofuata si kujenga tu, bali kuhakikisha uwekezaji wa Sh bilioni 3.17 katika Hospitali ya Mpitimbi unazalisha matokeo endelevu kwa wananchi.

Halmashauri ya Wilaya ya Songea inahitaji kufuatilia viashiria kama muda wa kusubiri mgonjwa, idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa, upatikanaji wa dawa na vifaa, muda wa rufaa, idadi ya upasuaji, vifo vya mama na mtoto, pamoja na kuridhika kwa wagonjwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Elizabeth Gumbo anasema miundombinu ya watumishi iliyojengwa jirani na hospitali imeboresha mazingira ya kazi na kusaidia upatikanaji wa huduma.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Elizabeth Gumbo.

Hatua inayofuata ni kuunganisha miundombinu hiyo, ajira, mafunzo endelevu, vifaa vinavyofanya kazi na mfumo wa rufaa unaopunguza ucheleweshaji kwa wananchi.

Sh bilioni 3.17 zinapimwa kwa maisha

Hospitali ya Mpitimbi sasa ina simulizi kubwa kuliko majengo yake; ni simulizi ya mwanamke anayejifungua bila kusafiri mbali, mtoto anayepata uchunguzi kwa wakati, mgonjwa anayefikiwa na daktari bingwa na familia inayookoa gharama za safari.

Hata hivyo, mafanikio yake ya kweli hayatapimwa kwa uzinduzi wala thamani ya fedha zilizotumika, bali yatapimwa kwa idadi kubwa ya wagonjwa wanaopata huduma salama kwa wakati na maisha yanayookolewa hivyo kupunguza idadi ya vifo vinavyotokea.



Wananchi wa Kijiji cha Kwamhuza, Kata ya Dakawa wilayani Mvomero wakifuatilia mada kuhusu ukatili wa kijinsia.

Ushirikina, umasikini unalea, kuchochea ukatili wa kijinsia

Na John Nditi

IMANI za kishirikina zinazidi kutajwa kama changamoto na moja ya vichocheo vikuu vya ukatili wa kijinsia, zikisaidiwa na umasikini miongoni mwa jamii.

Katika baadhi ya jamii imani hizo zinadaiwa kuchangia na kuchochea kufanyika kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, huku zikijenga hofu, mashaka na kutokuaminiana miongoni mwa wananchi.

Baadhi ya watu wanatumia imani hizo kama kisingizio cha kunyanyasa, kutishia, kubagua na hata kufanya ukatili huo dhidi watu wengine hususani wanawake, watoto na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi.

Tuhuma zinazohusishwa na imani za kishirikina zimekuwa zikisababisha vitisho, unyanyapaa, migogoro ya kifamilia na vitendo vya ukatili vinavyohatarisha maisha ya watu.

Hali hiyo imeibua haja ya kuongeza elimu kwa jamii kuhusu madhara ya imani potofu na umuhimu wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia bila kujali vinafanywa kwa kigezo au kisingizio gani.

Katika Kijiji cha Kwamhuza, Kata ya Dakawa wilayani Mvomero katika Mkoa wa Morogoro, imani hizo zinaelezwa kuwa miongoni mwa mambo yanayochangia vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuongeza hofu kwa wananchi.

Kutokana na hali hiyo, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Morogoro kupitia Mradi wa Girls With A Purpose (GWAP), hivi karibuni liliandaa mkutano wa kutoa elimu kuhusu namna ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wananchi wa Kijiji cha Kwamhuza na maeneo mengine.

Mkutano huo ulikuwa na kaulimbiu isemayo: “Sote Tuungane Kupinga Ukatili wa Kijinsia” ikibeba ujumbe maalumu: “Tumewekeza Nguvu katika Kupinga na Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia. Ukatili kwa Wanawake Sasa Basi, Ukatili kwa Watoto Sasa Basi, Ukatili Sasa Basi.”

Katika mkutano huo, wananchi wanasema baadhi ya matukio ya ukatili yanapotokea, wahusika hushindwa kutoa taarifa katika mamlaka husika kutokana na hofu ya vitisho kwamba watalogwa na watu wanaotuhumiwa kuhusika na vitendo hivyo.

Mmoja wa wakazi wa Dakawa, Magreth Pantaleo anasema watu wanaotekeleza vitendo vya ukatili wa kijinsia hufanya hivyo kwa malengo mbalimbali, yakiwemo madai ya kutumwa na baadhi ya watu au kudanganywa na waganga wa kienyeji kuwa watapata utajiri.

Anasema katika matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto, baadhi ya familia hushindwa kutoa taarifa kutokana na vitisho vinavyotolewa dhidi ya waathirika na ndugu zao.

Kwa mujibu wa Magreth, hali duni ya kiuchumi pia ni changamoto inayochangia baadhi ya familia kushindwa kufuatilia haki za waathirika, huku nyingine zikikubali kupokea fedha kutoka kwa watuhumiwa na kumaliza mashauri kifamilia, yaani nje ya mfumo wa kisheria.

Anasema hali hiyo huwaacha waathirika wakiwa na maumivu ya kisaikolojia, huku watuhumiwa wakikwepa kuwajibishwa kisheria na kuendelea kutekeleza vitendo hivyo.

“Changamoto za kiuchumi katika baadhi ya jamii zinachangia kufanyika kwa maamuzi ya kumalizana kienyeji katika matukio hayo kwa kupeana fedha za kujikimu,” anasema Magreth.



Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Morogoro, Mary Nnko akiwasilisha mada kuhusu ukatili wa kijinsia kwa wananchi wa Kijiji cha Kwamhuza, Kata ya Dakawa wilayani Mvomero.

Anasisitiza kuwa, utaratibu huo hunyima waathirika haki zao na kuacha makovu ya muda mrefu, huku sheria zikishindwa kufuatwa.

Naye Katibu wa Idara ya Wanawake na Watoto wa KKKT Dayosisi ya Morogoro, Mchungaji Dk Rhoda Chamshama anasema hakuna dini inayohalalisha ukatili katika jamii, hivyo wananchi wanapaswa kuungana kupinga vitendo hivyo.

“Ukatili wa kijinsia haukubaliki katika dini zote. Tuhakikishe tunapambana kutokomeza ukatili wa kijinsia katika makundi yote. Ukatili unaweza kumpata mtu yeyote bila kuangalia umri wala dini yake,” anasema.

Anasema kanisa linaungana na wadau mbalimbali, ikiwemo serikali katika juhudi za kutokomeza ukatili wa kijinsia kupitia utoaji wa elimu kwa jamii.

“Kanisa linapita ndani ya jamii kutoa elimu ili wananchi wapate uelewa kuhusu suala zima la ukatili wa kijinsia na hatua za kufuata pindi tukio la ukatili linapotokea,” anasema Mchungaji Dk Chamshama.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa GWAP, Yona Kitua anasema kanisa linatamani kuona jamii endelevu isiyo na vitendo vya ukatili.

Anasema amani na utulivu ni nguzo muhimu katika kuleta maendeleo.

Kitua ambaye pia ni Katibu wa Idara ya Mipango na Maendeleo wa KKKT Dayosisi ya Morogoro, anasema jamii yenye amani na utulivu huwa na mazingira mazuri ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Anahimiza wananchi na wanandoa kulinda uhusiano wao na kushughulikia migogoro ya kifamilia kwa njia zinazofaa, akieleza kuwa migogoro na kuvunjika kwa ndoa kunaweza kuongeza mazingira hatarishi kwa watoto. Kwa mujibu wa Kitua, baadhi ya watoto wanaoishi katika familia zenye migogoro hukumbana na changamoto za kisaikolojia, kukosa fursa za elimu na kushuka kwa kiwango cha ufaulu shuleni.

“Kuvunjika kwa ndoa na migogoro ya ndoa kunachangia kuongezeka kwa matukio ya ukatili kwa watoto. Wanaweza kukosa elimu, kuathirika kisaikolojia na kushindwa kufanya vizuri shuleni,” anasema Kitua.

Aidha, anasisitiza umuhimu wa wadau kushirikiana na kukemea imani potofu zinazoweza kutumiwa kama kichocheo cha vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Ofisa wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Jeshi la Polisi, Kituo cha Dakawa, Mwajuma Mkojola anasema vituo vya polisi ni sehemu salama kwa waathirika na watu wenye taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia kufikisha taarifa zao.

Anasema Jeshi la Polisi linazingatia usiri wa watoa taarifa ili kuwapa ujasiri wa kuripoti matukio bila hofu ya kufichuliwa na kuumbuliwa.

Kwa mujibu wa Mkojola, wanaume pia wamekuwa wakikumbana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kutoka kwa wenza wao lakini baadhi yao hushindwa kutoa taarifa kutokana na aibu na hofu.

Anasema hali hiyo husababisha baadhi ya wanaume kuendelea kunyanyasika ndani ya ndoa zao kwa kushindwa kutafuta msaada.

“Suala la ukatili wa kijinsia linapotokea kwa mtu yeyote, ama awe mwanamke, au mwanaume, linapaswa kutolewa taarifa polisi na hatua za kisheria zitachukuliwa,” anasema Mkojola.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Pelice Lumambo anazungumzia changamoto kubwa katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia, akisema ni baadhi ya wananchi kushindwa kutoa taarifa kwa wakati na tabia ya kuficha matukio hayo.

Anaomba wananchi wa Kijiji cha Kwamhuza na Wilaya ya Mvomero kwa ujumla kutoa taarifa za matukio yote ya ukatili wa kijinsia kwa mamlaka husika ili hatua stahiki zichukuliwe.

“Niwaombe wananchi wa kijiji hiki na Wilaya ya Mvomero kwa ujumla watoe taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia kwa mamlaka husika,” anasema Pelice.

Anasema utoaji wa taarifa kwa wakati utaiwezesha serikali kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watu wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Ofisa huyo anasema kufanya hivyo kutasaidia kupunguza na hatimaye kutokomeza ukatili katika jamii.

Pelice anasema serikali ya wilaya itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo, zikiwemo taasisi za dini, kutoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano na mikusanyiko mbalimbali ili kujenga uelewa kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia na umuhimu wa kuripoti matukio yake ya ukatili wa kijinsia.